**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**

*(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)*

*Email: ded.mkalamadc@singida.go.tz*

*Simu Na. 026-2964000*

***Unapojibu tafadhali taja***

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
P. O. Box. 1007,
**MKALAMA**

Kumb. Na. MDC/U.110/4/126 22/03/2018

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mara baada ya kupokea Kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb. Na. **CFC 26/205/01 "F"/91** cha tarehe **22/08/2017,** na Barua yenye Kumb. **CFC.26/205/01"GG" 95** ya tarehe **12/03/2018** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama anapenda kuwatangazia Wananchi wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi ya **Mtendaji wa Kijiji III** kwa Masharti ya kudumu. Nafasi hizo ni kama zinavyoonekana Katika mchanganuo ufuatao:-

**Mtendaji wa Kijiji Daraja III- (NAFASI 31)**

**i. Sifa za Kitaaluma kwa mwombaji**

- Awe amehitimu na kufaulu Elimu ya Kidato cha nne au Sita
- Aliepata mafunzo ya stadi za kazi ngazi ya Astashahada/Cheti **(NTA Level 5**) katika fani zifuatazo:-
  Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**ii. Mshahara**

Ngazi ya Mshahara wa awali ni **TGS B/1** sawa na Tshs **390,000/=** kwa mwezi.

**iii. Majukumu ya Mtendaji wa Kijiji**

a) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
b) Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora.
c) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Jamii
d) Katibu wa mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
e) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
f) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneeo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
g) Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika Kijiji
h) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
i) Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
j) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
k) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

## MASHARTI YA JUMLA YA MUOMBAJI KAZI

- Awe raia wa Tanzania
- Awe na umri wa miaka 18-45
- Awe hajawahi kufukuzwa kazi, kupunguzwa, kuachishwa au kustaafishwa kazi katika Utumishi wa Umma
- Kila mwombaji aambatanishe wasifu wake (CV) na picha ndogo 2 (*pasport size* )zilizopigwa hivi karibuni
- Kila mwombaji aandike kwa usahihi **anwani** yake na **namba ya simu** inayopatikana muda wote kwa ajili ya mawasiliano
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **08/04/2018 saa 9:30 Alasiri**
- Maombi yote yawasilishwe kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MKALAMA
S. L. P 1007
**SINGIDA**

Tangazo hili limetolewa na,

Eng. Godfrey T. Sanga
MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA
**MKALAMA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA

**Nakala:** -Mbao za Matangazo
-Tovuti ya Halmashauri